**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA TANZANIA**

# HOTUBA YA KAIMU MKURUGENZI WA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA DKT. KASSIMU A. NIHUKA KWENYE MKUTANO WA MWAKA WA WAKUFUNZI WAKAZI WA MIKOA TAREHE 8 – 9/05/2018, MAKAO MAKUU – DAR ES SALAAM

**KAIMU MKURUGENZI**

**MEI, 2018**

***Kaimu Naibu Mkurugenzi – Taaluma, Utafiti na Ushauri, Dkt. Honest Kipasika,***
***Kaimu Naibu Mkurugenzi – Mipango,Fedha na Utawala, Bi Mary Watugulu,***
***Mwenyekiti wa Wakufunzi wa Mikoa,***
***Wakuu wa Idara mliopo hapa,***
***Wakufunzi Wakazi wa Mikoa na Wakuu wa Kampasi,***
***Wakuu wa Idara na Vitengo,***
***Wageni waalikwa,***
***Mabibi na mabwana.***

***Habari za Asubuhi***

Awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutukutanisha tena katika mkutano wa mwaka wa wakufunzi wakazi wa mikoa pamoja na Wakuu wa Kampasi zetu za WAMO - Morogoro na Luchelele - Mwanza. Aidha, napenda niwapongeze wakufunzi wakazi wote pamoja na wakuu wa vituo kwa kazi kubwa mnayoendelea kuifanya katika vituo vyenu vya kazi. Nawasihi muendelee kufanya kazi kwa bidii kwa ustawi wa TEWW.

Napenda pia kuishukuru sekretarieti kwa maandalizi mazuri ya mkutano huu kwani fursa hii ni muhimu sana kwa kuwa inatukutanisha pamoja ili kutafakari, kutathimini na kuweka mikakati ya kuboresha utendaji katika vituo vyetu vya mikoa na TEWW kwa ujumla.

***Ndugu Washiriki,***

Ninafurahi kuhudhuria mkutano huu kwa mara ya tatu nikiwa TEWW, lakini mwaka huu nahudhuria nikiwa mtendaji mkuu baada ya aliyekuwa Mkurugenzi wetu Dkt. Fidelice Mafumiko kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali kuanzia tarehe 03.04.2018. Kwa niaba yenu, nampongeza sana Dkt. Mafumiko kwa uteuzi huo na Mungu amjalie afya njema,

hekima na Busara tele katika kutekeleza majukumu yake mapya. Napenda kuwahakikishia pia nitawapa ushirikiano ambao utasaidia kuijenga TEWW. inaweza kusonga mbele.

***Ndugu Washiriki,***

Nafahamu kuwa katika mkutano huu mtapokea taarifa mbalimbali na kuzijadili pamoja na kupendekeza maazimio kwa ajili ya utekelezaji.

Napenda kuwasisitiza kujadili kwa kina taarifa na mambo mbalimbali yatakayo wasilishwa na kutoa mchango chanya kwa maendeleo ya Taasisi yetu.

***Ndugu Washirik,***

Kufuatia changamoto zilizojitokeza miezi michache iliyopita kuhusiana na umuhimu wa TEWW na kama bado inahitajika katika jamii, napenda niwasihi kila mmoja wetu ajipange upya katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu majukumu ya TEWW, mafanikio yake changamoto na mipango ya baadaye. kila Mkufunzi Mkazi, Mkuu wa Kampasi, Wafanyakazi wote pamoja na wanafunzi ni lazima tuwe na uelewa mmoja kuhusu EWW. Nitumie nafasi hii kuwasihi kuwa mzingatie hili katika majadiliano yenu. Aidha mtenge muda wa kujadili majukumu ya TEWW Kisheria (Act. No. 12 of 1975) sambamba na kutafakari mafanikio yetu, changamoto na mipango yetu ya baadae.

***Ndugu Mgeni Rasmi,***

Kama unavyo fahamu, TEWW ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 12 ya mwaka 1975 ili kutekeleza majukumu mbalimbali yahusuyo elimu ya Watu Wazima nchini.

Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la wafanyakazi kuwa, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ilipendekeza kudurusu sheria hii. Kwa sasa, andiko la vipengele vilivyodurusiwa limewasilishwa kwenye ngazi husika baada ya kuidhinishwa na Bodi ya usimamizi ya TEWW. Maboresho yaliyopendekezwa yanalenga katika kufikia dira ya Taasisi ya kujenga jamii iliyoelimika na inayojiendeleza sawa na kaulimbiu ya TEWW ya “Elimu Haina Mwisho”.

Vile vile, Taasisi inafanya tathmini ya Mpango Mkakati wa sasa (2014/2015 – 2018/2019) kwa lengo la kudurusu ili uendane na mahitaji ya sasa ya kujenga Tanzania ya uchumi wa kati inayotegemea uchumi wa viwanda. Hata hivyo kwa sasa, tutaendelea kutumia Mpango Mkakati uliopo hadi hapo tutakapokamilisha kudurusu na kupata Mpango Mkakati mpya (2018/2019 – 2022/2023). Ni mategemeo yangu kuwa Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakufunzi Wakazi na Wakuu wa Kampasi wataendelea kuandaa “OPRAS” zao na kutekeleza majukumu yao kwa kutumia Mpango Mkakati wa sasa.

***Ndugu Washiriki,***

Katika juhudi za kujipambanua zaidi ili jamii na wadau mbalimbali wajue majukumu yetu tuliyoyatekeleza katika kila mwaka husika, Menejimenti ya TEWW imeunda timu mbili, moja ya kuandika “Annual Activity Report” ya TEWW kwa mwaka 2018/2019 na nyingine inaandika “Facts and Figures” ya TEWW ambayo itatoa takwimu mbalimbali za TEWW katika nyanja mbalimbali kuanzia ilipoanzishwa hadi 2018/2019. Viongozi wa Timu hizi mbili za kuandika nyaraka hizi za kimkakati zinaongozwa na Bw. Patrick Kisigiro na Bw. Celestine Magesa. Wajumbe wengine ni Mwajuma

Mohamed, Samweli Gasuku, Shabani Maijo, Elinaike Marti, Sylvester Mbumbe na Justine Mbwambo.

Ni matarajio yetu kuwa nyaraka hizi zitakamilika kwa wakati ili zianze kutumika kuanzia tarehe 1. Julai, 2018.

***Ndugu Washiriki,***

Kama mnavyofahamu kuwa awali mlipewa taarifa ya kusitishwa kwa zoezi la Usajili wa vituo vya elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi. Hata hivyo napenda kuwafahamisha kuwa Taasisi tumeruhusiwa kuendelea kusajili vituo hivi hadi hapo tutakapofahamishwa vinginevyo. Ni vema tuongeze umakini kwa kuhakikisha kuwa vituo vitakavyosajiliwa vinakidhi vigezo vilivyowekwa pamoja kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa mara kwa mara.

Sambamba na hili, tumeagizwa kupitia upya utoaji wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi hususani kipengele cha muda (miaka) ambao mwanafunzi anasoma kabla ya kuhitimu masomo yake. Hoja ni kuwa mwanafunzi anayesoma elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi anahitaji muda sawa na yule anayesoma katika mfumo rasimi au hata zaidi. Hivyo, kupitia ofisi ya Kaimu Naibu Mkurugenzi – Taaluma, Utafiti na Ushauri, Idara ya Elimu Masafa inaandaa andiko kuhusu hoja hiyo ili liwasilishwa kwenye vikao mbalimbali vya maamuzi ndani ya Taasisi. Taarifa zaidi zitatolewa baada ya kufikia maamuzi juu ya suala hilo.

***Ndugu washiriki;***

Ili kuendana na msimamo wa serikali ya awamu ya tano, menejimenti ya TEWW imedhamiria kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Taasisi pamoja na kuhakikisha yanaelekezwa katika kutekeleza malengo ya kipaumbele

ya Taasisi kadiri ya mpango kazi wa Taasisi na ule wa Vituo, Kampasi, Idara na Vitengo kwa ujumla. Katika kutekeleza hili, Wakufunzi Wakazi, Wakuu wa Kampasi na Mkuu wa Idara ya Mafunzo wanaagizwa kusimamia ukusanyaji wa ada kwa umakini mkubwa pamoja na kuhakikisha kuwa wanafunzi wale tu waliolipa ada ndio wanasajiliwa na kupata huduma katika vituo vyote. Pia, tumesambaza barua kwa Wakufunzi Wakazi ili wazifikishe kwa Wadau tuliowasajili kuendesha "Open Schools" ili walipe ada ya uratibu pamoja na kuhakikisha wanafuata taratibu za kuendesha "Open Schoos" kadiri ya miongozo ya TEWW. Kwa upande wetu Taasisi tutaendelea kuboresha huduma zetu kwa wadau ikiwa ni pamoja na kuwatembelea mara kwa mara na kutoa vyeti vya kuhitimu (Leaving Certificates) kwa wakati kuanzia Novemba, 2018 kwa kutumia mwongozo / mkakati ulioandaliwa na Idara ya Elimu Masafa.

***Ndugu Washiriki,***

Ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua stadi za kisomo nchini, TEWW imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (National Literacy and Mass Education Strategy) utakaoanza kutekelezwa kuanzia Julai, 2018. Kupitia Mkakati huu, Taasisi itafungua vituo vya kisomo katika mikoa 21 ya Tanzania bara ili kutoa fursa kwa vijana na watu wazima ili wapate fursa ya kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na kupata stadi za ujasiriamali na ufundi unaoendana na mazingira yao. Ili kufanikisha lengo hili, TEWW itatumia wanafunzi wetu wanaosoma Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Taasisi zilizopo WAMO - Morogoro, Dar es salaam na Luchelele - Mwanza pamoja na vijana wa kujitolea (volunteers) ambao watapatiwa mafunzo

maalumu.  Wito wetu kwa jamii ni kujitokeza ili kutumia fursa hii ya kisomo na wale wanaopenda kujitolea katika vituo vyetu wawasiliane na Wakufunzi Wakazi katika mkoa husika.

Baada ya maelezo haya, sasa natamka rasmi kuwa mkutano huu wa mwaka wa Wakufunzi Wakazi wa mikoa umefunguliwa rasmi.

***ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.***